# JARIDA LA KILIMO HIFADHI

**APRILI 2026 ● UJAZO NAMBA 12 ● NAKALA YA 1**

**NDANI YA TOLEO HILI**

UKUZAJI WA HARAKATI ZA KILIMO ENDELEVU NCHINI KENYA

Hadithi ya Mabadiliko Makubwa Zaidi: Safari Yenye Matumaini ya Kikundi cha Wafugaji Nyuki cha Babu, Mandhari ya Komto

Asili Katika Vitendo: Kujenga Mandhari na Maisha ya Kujikimu Yenye Ustahimilivu

Ratiba za Safari za ALTA



**Hadithi ya Kitovu cha Kilimo Hifadhi (KH) -Kenya**

## *UKUZAJI WA HARAKATI ZA KILIMO ENDELEVU NCHINI KENYA*

***John Mbae: Mshauri wa Kiufundi wa Kilimo na Maisha ya Kujikimu kwa Afrika Mashariki***

### UTANGULIZI

Jumuiya ya Utekelezaji wa Maarifa (Community of Practice – CoP) huwaleta pamoja wakulima, wataalamu, watafiti, na wadau wengine wenye lengo la pamoja la kuboresha mifumo ya kilimo na maisha ya kujikimu. Kupitia mwingiliano wa mara kwa mara iwe ni katika mikutano, ziara za mashambani, au majukwaa ya kidijitali wanachama hubadilishana uzoefu, kutatua changamoto kwa pamoja, na kujenga juu ya maarifa ya kila mmoja. Katika sekta ya kilimo, ambako hali hubadilika kila wakati kutokana na mabadiliko ya tabianchi, masoko, na ubunifu, Jumuiya ya Utekelezaji wa Maarifa (CoP) hutoa nafasi ya vitendo kwa ajili ya kujifunza endelevu, kujirekebisha, na kushirikiana, hivyo kusaidia jamii kuondoka kwenye juhudi za pekee kuelekea hatua zilizo shirikishi na zenye athari kubwa zaidi.

Canadian Foodgrains Bank
A Christian Response to Hunger

**Washauri wa Kiufundi wa Kilimo na Maisha wa Canadian Foodgrains Bank**

**John Mbae** john.mbae@tearfund.org | jkirima@foodgrainsbank.ca
**Nester Mashingaidze** nmashingaidze@foodgrainsbank.ca
**Jean Twilingiyumukiza** jean.twilingiyumukiza@tearfund.org | jtwilingiye@foodgrainsbank.ca
**Lilian Zheke** lilian.zheke@tearfund.org | lzheke@foodgrainsbank.ca

Katika maeneo kame na jamii za wakulima nchini Kenya, athari za mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa udongo, na mvua zisizotabirika zinaonekana wazi zaidi. Wakulima wanakabiliwa na changamoto za kupungua kwa rutuba ya udongo, kuongezeka kwa gharama za uzalishaji, na mabadiliko ya mifumo ya hali ya hewa yanayotishia maisha yao ya kujikimu. Hata hivyo, katikati ya changamoto hizi, kuna harakati inayokua kwa kasi inayowasaidia wakulima kujenga upya uimara na kurejesha afya ya udongo wao Kitovu cha Kilimo Hifadhi Kenya (CA-Kenya Hub).

## DIRA ILIYOANZA KWA USHIRIKIANO

Hadithi ya Kitovu cha Kilimo Hifadhi (KH) Kenya ilianza mwaka 2011, pale kundi dogo la mashirika lilipokusanyika kwa pamoja likiwa na dira moja: kukuza Kilimo Hifadhi kama njia ya kufikia uzalishaji endelevu wa chakula nchini Kenya.

Mpango huu ulipata msaada wa awali kutoka Benki ya Chakula ya Nafaka ya Kanada (Canadian Foodgrains Bank), ukiwaleta pamoja washirika wa kimataifa wakiwemo Kamati Kuu ya Shirika la Mennonite (Mennonite Central Committee -MCC), Huduma za Shirika la Baptist la Kanada (Canadian Baptist Ministries -CBM), Shirika la Msaada wa Kibinadamu Duniani la Kanada (World Relief Canada (sasa Tearfund Canada), Shirika la Urejeshaji na Maendeleo ya Jamii Duniani ( World Renew), na ADRA, pamoja na mashirika ya Kenya kama vile Baraza la Kitaifa la Makanisa ya Kenya (NCCK), Shirika la Maendeleo la Utooni (UDO), na Suluhisho la Sahel (Sahelian Solutions - SASOL).

## MTANDAO UNAOKUA KWA KASI

Kwa miaka mingi, Kitovu cha Kilimo Hifadhi Kenya (CA-Kenya) kimeendelea kupanua wigo wake na ushawishi wake. Kutoka kundi la awali la mashirika manane waanzilishi, kitovu hiki kimekua na kuwa mtandao hai unaojumuisha sasa washirika wapya wa taasisi, wadau wa serikali, taasisi za utafiti, sekta binafsi, washirika wa maendeleo, mashirika ya wakulima, pamoja na wataalamu binafsi wenye shauku ya kuendeleza kilimo endelevu. Leo, jamii ya Kitovu cha Kilimo Hifanya Kenya (CA-Kenya Hub) imekua na kufikia zaidi ya washirika 15 na wanachama binafsi zaidi ya 184, jambo linaloonyesha kuongezeka kwa hamasa na dhamira ya kitaifa katika kukuza Kilimo Hifadhi nchini Kenya. Ukuaji huu umeimarisha uwezo wa kitovu katika kubadilishana maarifa, kuratibu programu, na kuongeza athari za mipango ya kilimo endelevu kote nchini.

Kitovu hiki kinasimamiwa na Mtandao wa Afrika wa Kilimo Hifadhi Ardhi (Africa Conservation Tillage Network – ACTN) katika KALRO Kabete, Nairobi, na kinaendelea kuwa sehemu ya kukutanisha mashirika yanayofanya kazi kubadilisha mifumo ya kilimo nchini Kenya kupitia mbinu za Kilimo Himilivu kwa Mabadiliko ya Tabianchi (Climate Smart Agriculture).

## KUJIFUNZA, KUSHIRIKISHANA, NA KUPANUA SULUHISHO

Katika kipindi cha zaidi ya muongo mmoja uliopita, Kitovu cha Kilimo Hifadhi Kenya (CA-Kenya) kimejenga jumuiya imara ya utekelezaji wa maarifa (Community of Practice) inayozunguka Kilimo Hifadhi mbinu inayozingatia kanuni tatu kuu: kuvuruga udongo kwa kiwango kidogo; kuwa na ufunikaji wa kudumu wa udongo; na mzunguko wa mazao. Mbinu hizi huwasaidia wakulima kurejesha rutuba ya udongo, kuongeza uzalishaji, kupunguza nguvu kazi, na kujenga ustahimilivu dhidi ya mishtuko ya mabadiliko ya tabianchi.

Kupitia mikutano ya mara kwa mara, matukio ya mafunzo, na ubadilishanaji wa maarifa, Kitovu hiki kimewezesha washirika kushirikishana uzoefu na kuimarisha programu zao kote nchini Kenya. Hatua muhimu ilikuwa ni Mkutano wa Kilimo Hifadhi Kenya uliofanyika mwaka 2018 na Kongamano la Kitaifa la Kilimo Hifadhi Kenya lililofanyika mwaka 2025, lililoandaliwa na kitovu hiki, ambalo liliwaleta pamoja wadau wa kitaifa na kimataifa ili

kuendeleza ajenda ya Kilimo Hifadhi na kuimarisha ushirikiano. Wakati wa kongamano hilo, baadhi ya vinara wa Kilimo Hifadhi walitambuliwa kwa kazi yao bora katika kukuza na kutekeleza mbinu hizi.

Tangu hapo, wanachama wa Kitovu wameendelea kutekeleza mipango ya Kilimo Hifadhi katika kaunti mbalimbali, wakifikia maelfu ya wakulima na kusaidia jamii kupokea na kutumia mbinu endelevu zaidi za kilimo.

## KUKABILIANA NA MABADILIKO YA MANDHARI YA KILIMO

Kadri sekta ya kilimo nchini Kenya inavyoendelea kubadilika, ndivyo pia jukumu la Kitovu cha Kilimo Hifadhi Kenya (CA-Kenya) lilivyobadilika. Ugatuzi umeongeza nafasi ya serikali za kaunti katika sekta ya kilimo, huku mabadiliko ya tabianchi yakiongeza uhitaji wa mifumo ya kilimo iliyo imara na yenye ustahimilivu.

Kwa kutambua mabadiliko haya, Kitovu kiliandaa Mpango Mkakati wa 2023–2026, unaotoa mwongozo wa kuimarisha ushirikiano na kupanua wigo wa Kilimo Hifadhi.

Mkakati huu unalenga vipaumbele vitano vikuu:

- Kueneza Kilimo Hifadhi: Kusaidia wakulima kupitia mafunzo, maeneo ya majaribio (demonstration sites), na programu za uhamasishaji ili kuongeza utumiaji wa mbinu za Kilimo Hifadhi.
- Kuimarisha Utafiti na Uwezo: Kushirikiana na vyuo vikuu na taasisi za utafiti ili kuzalisha ushahidi, kuendeleza ubunifu, na kujenga kizazi kijacho cha wataalamu wa Kilimo Hifadhi;
- Utetezi na Ushiriki katika Sera: Kufanya kazi na serikali ya kitaifa na za kaunti ili kuingiza Kilimo Hifadhi katika sera za kilimo na mipango ya maendeleo;
- Mawasiliano na Ubadilishanaji wa Maarifa: Kupanua majukwaa ya kidijitali, ushiriki wa vyombo vya habari, na rasilimali za kujifunzia ili kuongeza uelewa wa ubunifu na mafanikio ya Kilimo Hifadhi;
- Uhamasishaji wa Rasilimali: Kujenga ushirikiano na kupata uwekezaji ili kuunga mkono ukuaji wa muda mrefu na uendelevu wa Kitovu.

## “WAKULIMA KATIKA KITOVU”

Kiini cha kazi ya Kitovu cha Kilimo Hifadhi Kenya ( CA-Kenya) ni wakulima na jamii za vijijini. Kilimo Hifadhi kinatoa mbinu ya vitendo na inayofikika kirahisi, inayolingana kwa karibu na maarifa ya jadi ya kilimo huku ikiingiza ubunifu unaoboresha uzalishaji na utunzaji wa mazingira.

***“Inatia moyo kuona jinsi Kitovu cha Kilimo Hifadhi Kenya (CA Kenya) kilivyokua kwa miaka hadi kuwa jukwaa hai la ushirikiano na ubadilishanaji wa maarifa. Nguvu yake ipo katika kujitolea kwa wanachama wake na thamani ya pamoja wanayoipata kwa kufanya kazi pamoja ikionyesha kuwa hatua za pamoja zina nguvu zaidi kuliko kufanya kazi peke yako.” Stephan Lutz, mwanzilishi/mwanzo wa Kitivo cha Kilimo Hifadhi (CA Hub) na mwenyekiti wa zamani.***

***“Kitovu cha Kilimo Hifadhi” (CA Hub), kwa kuwaleta pamoja wadau mbalimbali, inatambua athari ya kuongezeka (multiplier effect) ya ushirikiano katika kupanua Kilimo Hifadhi” Dkt. Boaz Waswa, Mwenyekiti wa sasa wa Kitovu.***

Kwa wakulima wengi wadogo, kutumia mbinu za Kilimo Hifadhi kumemaanisha kuwa na udongo wenye afya bora zaidi, mavuno yanayotegemewa zaidi, na kuimarika kwa usalama wa chakula katika kaya.

## MTAZAMO WA MBELE / MUSTAKABALI

Safari ya Kitovu cha Kilimo Hifadhi Kenya ( CA-Kenya) inaonesha nguvu ya ushirikiano katika kukabiliana na changamoto tata za kilimo. Kwa kuwaleta pamoja washirika wenye mitazamo na mifumo tofauti ya maarifa, kitovu hiki kinasaidia kujenga mustakabali wa kilimo ulio imara na wenye ustahimilivu nchini Kenya.

Kadri mtandao unavyoendelea kukua, dira yake inaendelea kuwa wazi: Kenya yenye uhakika wa chakula, inayoungwa mkono na mifumo ya kilimo inayostahimili mabadiliko ya tabianchi. Ukuaji wa mpango huu umechochea kuongezeka kwa hamasa katika sekta mbalimbali kuhusu kilimo himilivu kwa mabadiliko ya tabianchi, ikiwa ni pamoja na suluhisho zinazotegemea asili (nature-based solutions), agroikolojia, kilimo rejelevu (regenerative agriculture), Mbinu ya Kilimo inayozingatia kanuni za Mungu na uhifadhi wa udongo (*Farming God’s Way)*, na uhifadhi wa udongo na maji, miongoni mwa nyingine.

Kupitia ushirikiano, ubunifu, na mbinu zinazomweka mkulima katikati, Kitovu cha Kilimo Hifadhi Kenya (CA-Kenya) hakibadilishi tu mbinu za kilimo bali kinakuza harakati ya kilimo endelevu itakayowanufaisha vizazi vijavyo:

- **Kupanua uanachama na utofauti:** Kuwakaribisha wakulima zaidi, vijana, watafiti, na wadau wa sekta binafsi ili kuimarisha ujifunzaji na ubunifu ndani ya mtandao.
- **Kuimarisha ubadilishanaji wa maarifa:** Kuendeleza majukwaa ya mara kwa mara ya ana kwa ana na ya kidijitali kwa ajili ya kushirikishana uzoefu wa vitendo, mafunzo yaliyopatikana, na mbinu bora zinazojitokeza katika Kilimo Hifadhi.
- **Kuweka kumbukumbu na kushirikisha athari:** Kukusanya hadithi za mafanikio, takwimu, na ushahidi ili kuonesha thamani ya kazi na kuvutia msaada zaidi.
- **Kukuza ubunifu:** Kuhamasisha majaribio ya teknolojia na mbinu zinazofaa mazingira ya ndani ili kukabiliana na changamoto mpya.
- **Kuhakikisha uendelevu:** Kuandaa mikakati ya muda mrefu ya umiliki, uhamasishaji wa rasilimali, na mwendelezo wa Jumuiya ya Utekelezaji wa Maarifa hata baada ya miradi kukamilika.

“Hadithi ya Kitovu cha Kilimo Hifadhi (CA Hub) ni ya dira ya pamoja na hatua za pamoja ambapo ushirikiano hubadilisha mawazo kuwa matokeo halisi, na ujifunzaji huwa msingi wa mabadiliko ya kudumu.”

### CHANZO:

Mpango Mkakati wacha Kilimo Hifadhi Kenya  (CA Hub Kenya) 2016–2018

Mpango Mkakati wa Kitivo cha Kilimo Hifadhi Kenya (CA Hub Kenya) 2023–2026

# Hadithi ya Mabadiliko Makubwa Zaidi: Safari Yenye Matumaini ya Kikundi cha Wafugaji Nyuki cha Babu, Mandhari ya Komto

***Tajebe Dibaba: Climate Resilience Manager (Food for the Hungry Ethiopia)***



Katika mandhari ya Komto nchini Ethiopia, mabadiliko ya kimya lakini yenye nguvu yanaendelea miongoni mwa wanachama wa Kikundi cha Wazalishaji Asali cha Babu. Kwa msaada wa Shirika la misaada ya chakula kwa wenye uhitaji nchini Ethiopia (Food for the Hungry Ethiopia kwa kushirikiana na Kamati Kuu ya Shirika la Mennonite Kanada (Mennonite Central Committee Canada), kikundi hiki chenye wanachama 14 wanawake 8 na wanaume 6 kinabadilisha maisha ya kujikimu kupitia ufugaji nyuki endelevu chini ya mpango wa asili (Nature+).

Mwanzoni, kikundi kilitegemea mizinga ya asili midogo, isiyo na ufanisi, na mara nyingi ikiwekwa juu ya miti. Kuvuna asali kulikuwa na hatari na kulihitaji nguvu kazi kubwa, huku mavuno yakiwa madogo. Ukosefu wa vifaa vya kujikinga uliwazuia pia baadhi ya wanachama kushiriki kikamilifu, hasa wanawake na wale walio katika mazingira magumu zaidi.

Kwa kutambua changamoto hizi, msaada maalum ulitolewa. Wanachama walipatiwa mafunzo ya vitendo kuhusu ufugaji nyuki wa kisasa, uzalishaji wa asali, uchakataji, na masoko, yakiratibiwa na wataalamu kutoka Kituo cha Utafiti wa Ufugaji Nyuki cha Holeta. Sambamba na hilo, kikundi kilipatiwa mizinga ya kisasa, vifaa vya kujikinga, na zana muhimu za ufugaji nyuki hivyo kuunda mazingira salama na jumuishi zaidi ya kazi.

Athari zimekuwa kubwa. Kwa kuboresha ujuzi na vifaa, kikundi kiliweza kuanzisha kituo cha uzalishaji wa asali (kibanda) na kuanza kuweka akiba kwa pamoja, kikikusanya birr 12,000 (fedha ya Ethiopia) - (sawa na CAD 105) kusaidia shughuli zao. Zaidi ya uzalishaji, kikundi hukutana mara kwa mara kujadili changamoto za kijamii, kuchangia mfuko wa pamoja, na kuimarisha ushirikiano miongoni mwa wanachama.

Kupitia safari hii, wanachama wamepata zaidi ya kipato wamejenga kujiamini, wameendeleza utaalamu wa kiufundi katika usimamizi wa makundi ya nyuki, na kugundua fursa mpya. Baadhi yao wameanza hata kuanzisha miradi yao ya ufugaji nyuki katika ngazi ya kaya.

Kwa sasa, kikundi kinajiandaa kusambaza mzigo wake wa kwanza wa asali bora kwenye soko kuu, kikizingatia viwango vinavyoongozwa na msaada wa kiufundi unaoendelea kutoka Kituo cha Utafiti wa Ufugaji Nyuki cha Holeta. Ushirikiano huu, ukiwemo mafunzo ya vitendo na ziara za ufuatiliaji, umeimarisha ubora wa bidhaa pamoja na uendelevu wa muda mrefu.

Kwa kuangalia mbele, Kikundi cha Wazalishaji Asali cha Babu kinaelekeza nguvu zake katika ukuaji. Mipango inaendelea kuongeza idadi ya mizinga ya kisasa, kuboresha kituo chao cha uzalishaji (kuezeka kibanda kwa mabati), na kupanua shughuli kwa kuingiza ufugaji wa kisasa wa kunenepesha mifugo. Kazi yao si tu inaboresha maisha ya kujikimu, bali pia inachangia urejeshaji wa mazingira kupitia uchavushaji ulioimarishwa na kuongezeka kwa bioanuwai.

Kama anavyosema Birhane Hambisa (mjumbe wa kamati): “Licha ya changamoto tulizokutana nazo kufika hapa, sasa tumeanza kuvuna asali bora.”

Hadithi hii ni ushahidi wa nguvu ya maarifa, ushirikiano, na suluhisho zinazotegemea asili ikionyesha jinsi jamii zinavyoweza kurejesha mifumo ya ikolojia huku zikijenga maisha ya kujikimu yaliyo imara na jumuishi.

---

## Asili Katika Vitendo: Kujenga Mandhari na Maisha ya Kujikimu Yenye Ustahimilivu

***Ndani ya Safari ya Fadhili Trust ya Kurejesha Mifumo ya Ikolojia na Kuwezesha Jamii Kibwezi***

### MUHTASARI

Kwa zaidi ya miaka 22, Wakfu wa Fadhili (Fadhili Trust) umekuwa ukishirikiana bega kwa bega na jamii nchini Kenya, ukihamasisha maisha ya kujikimu endelevu, ujumuishaji wa kifedha, na kilimo kinachostahimili mabadiliko ya tabianchi. Kilichoanza kama mpango wa huduma za nyumbani kimekua na kuwa shirika la kuaminika la ngazi ya jamii, likifanya kazi kwa karibu na makanisa, viongozi wa eneo, na vikundi vya wakulima ili kuleta mabadiliko ya kudumu.

Tangu mwaka 2018, Fadhili imeimarisha juhudi zake katika Kibwezi Magharibi, Kaunti ya Makueni, ambapo inasaidia jamii kupitia Vikundi vya Akiba na Mikopo ya Kijiji (VSL), Kilimo Hifadhi (CA), na hivi karibuni, urejeshaji wa mandhari unaozingatia asili (nature-positive landscape restoration). Wanawake wanaounda asilimia 90 ya wanachama wa Vikundi vya Akiba na Mikopo vya Kijiji (VSL) ndio kiini cha mabadiliko haya, wakimarisha ustahimilivu wa kaya pamoja na uongozi wa jamii.

***Hadithi ya Mafanikio katika Urejeshaji: Chemchemi Yarudi Uhuishaji wa Asili Kibwezi Magharibi: Jinsi juhudi za urejeshaji zinavyorejesha maji, uhai, na matumaini kwa jamii (inasimuliwa na Andy Mkurugenzi Mtendaji, CFGB)***



*Andy  Mkurugenzi Mtendaji wa CFGB katika chemchemi iliyorejeshwa*

Katika mandhari kame ya Kibwezi Magharibi, Kenya, maji yamekuwa rasilimali adimu siku zote, yakichagiza maisha na shughuli za kujikimu za jamii zinazoishi katika eneo hili. Kwa miaka mingi, chemchemi iliyosahaulika ilifichwa chini ya ardhi iliyoharibika maji yake yakitoweka, na uwepo wake kubaki kuwa kumbukumbu tu kwa wakazi wa zamani.

Leo, hadithi hiyo imebadilika. Akiwa amesimama katika eneo hilo, Andy, Mkurugenzi Mtendaji wa CFGB, anaelezea mabadiliko ya ajabu: chemchemi iliyopotea miongo kadhaa iliyopita imerudi tena ikitiririka upya baada ya miaka ya kazi za urejeshaji chini ya Mradi wa asili (Nature+).

Miaka minne tu iliyopita, mandhari hii ilikuwa na sura tofauti kabisa. Milima ilikuwa wazi bila uoto, udongo ukiwa umeachwa wazi, na mfumo wa ikolojia ukihangaika chini ya shinikizo la mmomonyoko wa udongo na ukame wa muda mrefu. Hakukuwa na uoto wa kutosha kuhifadhi unyevunyevu, wala kifuniko cha kusaidia mzunguko wa mvua, na hakukuwa na dalili yoyote ya chemchemi iliyowahi kusaidia jamii. Hata hivyo, kupitia juhudi za makusudi za urejeshaji kupanda upya mimea, kulinda ardhi, na kuruhusu asili kujirejesha kitu cha ajabu kilianza kutokea.

Kadri uoto ulivyorejea, ndivyo pia uwiano wa mfumo wa ikolojia ulivyorejea. Kisha, chemchemi ikajitokeza tena. Kilichokuwa ardhi kavu sasa ni chanzo muhimu cha maji, kinachotoa maji safi yaliyopimwa kwa ajili ya kunywa, umwagiliaji, na matumizi ya nyumbani. Kwa jamii, hii si chemchemi tu ni tegemeo la maisha.

“Hiki ndicho kinachotokea tunapoipa asili nafasi ya kujirejesha,” anaeleza Andy. “Mifumo ya ikolojia inapofufuliwa, haiungi mkono mazingira pekee bali pia inaendeleza maisha ya watu.” Urejeshaji huu wa Kibwezi Magharibi ni ukumbusho wenye nguvu kwamba hata mandhari zilizoharibika sana zinaweza kurejeshwa. Kwa mbinu sahihi na ushiriki imara wa jamii, asili inaweza kupona na inapopona, hurejesha kwa wingi.

## ATHARI KWA PICHA FUPI

Kazi ya Wakfu wa Fadhili imeleta matokeo yanayopimika kwa kiwango kikubwa:

- Wanachama zaidi ya 50,000 wameshiriki katika Vikundi vya Akiba na Mikopo ya Kijiji
- Vikundi zaidi ya 2,200 vya akiba vimeanzishwa
- Zaidi ya Dola za Marekani milioni 2.5 zimekusanywa kama akiba ya jamii
- Wakulima 5,596 wamepata mafunzo ya Kilimo Hifadhi, kati yao 4,071 wanatekeleza kikamilifu
- Wachungaji 96 na viongozi 368 wa makanisa na vijiji wamewezeshwa kuongoza mabadiliko ya jamii
- Mabingwa 120 wa masuala ya jinsia wamepata mafunzo ya uhamasishaji na utetezi dhidi ya ukatili wa kijinsia (GBV)

## MRADI WA MBINU ZA ASILI: SURA MPYA KATIKA UREJESHAJI WA MANDHARI

Ikiwa ni mwendelezo wa msingi huu imara, Wakfu wa Fadhili (Fadhili Trust) ilizindua mradi wa mifumo ya chakula inayozingatia asili (Nature+) katika mandhari ya Mbui Nzau eneo lililoathiriwa kwa kiasi kikubwa na ukame, mmomonyoko wa udongo, kupotea kwa bioanuwai, na kupungua kwa uzalishaji wa kilimo.

Mradi wa mifumo ya chakula inayozingatia asili  unawakilisha mbinu thabiti na jumuishi inayounganisha urejeshaji wa mazingira na mifumo ya chakula pamoja na maisha ya kujikimu, ukionyesha kuwa maendeleo endelevu yanafanikiwa zaidi pale ambapo binadamu na asili vinastawi kwa pamoja.

## KUTOKA UHARIBIFU HADI UREJESHAJI



Mandhari ya Mbui Nzau, Oktoba 2024



Picha iliyopigwa katika eneo hilohilo mwezi Mei 2025

Katika mandhari yote ya Mbui Nzau, mabadiliko yanayoonekana yako katika hatua ya utekelezaji. Jamii zinashiriki kikamilifu katika kurejesha mifumo ya ikolojia iliyoharibika kupitia suluhisho za vitendo zinazoendeshwa na jamii zenyewe, ikiwa ni pamoja na:

- Matuta ya udongo ya nusu duara (semi-circular bunds) ili kuboresha uhifadhi wa maji
- Gabioni kudhibiti mmomonyoko wa mifereji (gully erosion) na kuimarisha ardhi.

Katika mandhari yote ya Mbui Nzau, mabadiliko yanayoonekana yanaendelea. Jamii zinashiriki kikamilifu katika kurejesha mifumo ya ikolojia iliyoharibika kupitia suluhisho za vitendo zinazoendeshwa na mazingira ya ndani, ikiwa ni pamoja na:

- Matuta ya udongo ya nusu duara ili kuboresha uhifadhi wa maji.
- Vikasha au vikapu vya waya wa chuma vinavyojazwa na mawe, kokoto, au vifusi (Gabioni) kudhibiti mmomonyoko wa mifereji na kuimarisha ardhi.
- Urejeshaji wa maeneo dhaifu kama mfumo wa mifereji wa Kalamba.
- Urejeshaji wa milima ya Mbui Nzau kupitia kuzuia mifugo, upandaji miti, pamoja na uhifadhi wa udongo na maji

Hatua hizi si tu zinarejesha hali ya ardhi iliyoharibika, bali pia zinajenga upya msingi wa rasilimali asilia ambao jamii hutegemea kwa ajili ya maisha yao.

## KILIMO HIMILIVU KWA MABADILIKO YA TABIANCHI KWA MAISHA YA KUJIKIMU YENYE USTAHIMILIVU

Katika ngazi ya shamba, Mradi wa Nature+ unakuza mbinu za kilimo himilivu kwa mabadiliko ya tabianchi na kilimo rejelevu zinazoongeza uzalishaji huku zikilinda mazingira. Wakulima wanatekeleza:

- Mbinu za Kilimo Hifadhi
- Bustani za nyumbani (kitchen gardens) ili kuboresha lishe ya kaya
- Mbinu bunifu kama matumizi ya Azolla (mmea wa majini unaotumika kama chakula cha mifugo) au kwa ajili ya rutuba ya udongo na chakula cha mifugo.

Kupitia mashamba darasa (demonstration plots) na mifumo ya kujifunza ya wakulima, jamii zinapata maarifa na kujiamini kuhamia katika mifumo ya kilimo iliyo endelevu na yenye ustahimilivu zaidi.

## JAMII ZIKIWA KATIKATI

Nguvu kuu inayotofautisha Mradi wa Asili (Nature+) ni mfumo wake wa utawala unaoongozwa na jamii, unaohakikisha umiliki na uendelevu wa muda mrefu. Miundo iliyopo ni pamoja na:

Kamati za Ufuatiliaji wa Mradi katika ngazi ya kata; Kamati za Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya kitongoji; Vyama vya Watumiaji wa Maji na kamati za maeneo ya vyanzo vya maji (watershed); pamoja na mitandao ya wajitolea wa jamii waliopata mafunzo, wakiwemo wakulima vinara, mawakala wa VSLA, na mabingwa wa mazingira.

Mfumo huu jumuishi unaimarishwa kupitia ushirikiano na wadau wa serikali za kaunti na kitaifa, na hivyo kujenga mfumo imara wa uwajibikaji na upanuzi wa athari.

## IMANI KATIKA VITENDO: KUENDESHA MABADILIKO

Mbinu ya Fadhili Trust ya Mabadiliko ya Kanisa na Jamii (CCT) inaendelea kuwa na mchango mkubwa katika kuhamasisha mabadiliko. Makanisa si sehemu za ibada tu, bali pia ni vitovu vya maendeleo yakiiwezesha jamii:

- Kupanda miti na kutunza mazingira
- Kusaidia kaya zilizo katika mazingira magumu, wakiwemo wazee na yatima
- Kuanzisha vikundi vya akiba na kutumia mbinu za kilimo endelevu
- Kuwalea na kuwaongoza vijana katika uhifadhi na huduma kwa jamii

Muunganiko huu wa imani na maendeleo umeimarisha mshikamano wa kijamii na kuhamasisha hatua za pamoja katika ngazi ya jamii.

## USHIRIKIANO KWA ATHARI ENDELEVU

Katika msingi wake, mafanikio ya Wakfu wa Fadhili (Fadhili Trust) na Mradi wa Asili (Nature+) anatokana na ushirikiano. Kwa kuwaleta pamoja jamii, viongozi wa dini, taasisi za serikali, na washirika wa maendeleo, mpango huu unatumia nguvu ya ushirikiano ili kupanua athari.

## MTAZAMO WA MBELE / MUSTAKABALI

Kadri Mradi wa Asili (Nature+) unavyoendelea kukua, dira iko wazi: kupanua urejeshaji wa mandhari, kuimarisha utekelezaji wa kilimo himilivu kwa mabadiliko ya tabianchi, na kuzijenga mifumo ya jamii inayodumisha mabadiliko.
Wakfu wa Fadhili (Fadhili Trust) inaonesha kwamba pale jamii zinapowezeshwa, mifumo ya ikolojia inaporejeshwa, na ushirikiano kuimarishwa, mabadiliko hayawezekani tu bali pia ni endelevu.

# RATIBA ZA SAFARI ZA ALTA

**Jean Twiringiyumukiza:**

10–22 Aprili
N'Djamena, Chad & Kousseri, Cameroon
Tathmini ya CLWR-UFE na Warsha ya Mafunzo kwa Washirika

29–30 Aprili
Burera & Ngoma, Rwanda
Ziara ya CFGB na ziara ya kubadilishana uzoefu ya Wahaiti katika PDN & AEBR

04–08 Mei
Kigali, Rwanda
Warsha ya Kubadilishana Uzoefu wa Ufuatiliaji na Tathmini (M&E) ya CFGB

22–26 Juni
N.d, Rwanda
Kikao cha Kuhuisha Maarifa kwa Wakufunzi Wakuu (Master Trainers) wa Rwanda

**Lilian Zheke:**

20–24 Aprili
Mponela, Malawi
Kikao cha 3 cha Mafunzo ya Wakufunzi (MT), washirika wa Malawi

5–6 Mei
Masvingo, Zimbabwe
Warsha ya ngazi ya nchi, washirika wa Zimbabwe

8–12 Juni
Mponela, Malawi
Kikao cha 4 cha Mafunzo ya Wakufunzi (MT), washirika wa Malawi

**John Mbae:**

30–4 Aprili 2026
Tharaka Nithi, Kenya
Mafunzo kwa NCCK

7–10 Aprili 2025
Mwingi, Kenya
Mafunzo kwa ACC&S

13–17 Aprili 2026
Kibwezi, Kenya
Ziara ya Kubadilishana Uzoefu ya Nature Plus CoP

Mei/Juni 2026
Uganda
Warsha ya ngazi ya nchi

Mei/Juni 2026
Tharaka, Kenya
Warsha ya Mtandao wa Kitaifa

**Nester Mashingaidze**

Mei/Juni 2026
Uganda
Warsha ya Mtandao wa Ngazi ya Nchi

1–6 Juni 2026
Kenya
Mkutano wa Washirika wa Asili (Nature+)